REPUBLIC OF RWANDA

MINISTRY OF EDUCATION

REB
Rwanda Education Board

CURRICULUM FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT

# MUHTASARI WA SOMO LA KISWAHILI
# KIDATO CHA 4-6 Mchepuo wa lugha

DIGNITY AND NATIONAL IDENTITY

Januari 2015

# MUHTASARI WA SOMO LA KISWAHILI KIDATO CHA 4-6

## Mchepuo wa lugha

## Januari 2015

© 2015   Bodi ya Elimu Rwanda.

Haki zote zimehifadhiwa.

Muhtasari huu ni mali ya Bodi ya Elimu Rwanda .Shukrani ziwaendee waandishi  na  vyanzo vyake   wakati  wa  kuinukuu**.**

## DIBAJI

Bodi ya Elimu Rwanda inayo heshima kubwa kutoa mtaala mpya wa somo la Kiswahili kwa wadau wote. Mtaala huu ndio nyaraka rasmi itakayoongoza ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari nchini Rwanda. Mtaala huu umezingatia aina ya mtaala uegemeao katika kujenga ujuzi wa mwanafunzi (Mtaala Uegemeao Katika Ujuzi). Hivyo, mtaala huu unatoa mwongozo wa namna ya ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili kuendana na aina hii ya mtaala. Hii itasaidia kuhakikisha kwamba kuna kuwa na aina moja ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika nchi nzima.

Mtaala huu umezingatia falsafa ya elimu nchini Rwanda ambayo inalenga kuhakikisha kuwa vijana katika kila kiwango cha elimu wanafanikiwa kufikia kilele cha uwezo wao kuhusiana maarifa sahihi, ujuzi, stadi sahihi na mwenendo mwema wa tabia muafaka ambao unawajenga na kuwajumuisha katika jamii na waweze kuzitumia vilivyo fursa za ajira zilizopo. Ili kuhakikisha kuwepo kwa ubora wa elimu, mtaala huu umeweka mkazo katika kuhakikisha kuwa mikabala ya mtaala, ufundishaji na ujifunzaji na mikabala ya kiupimaji inafungamanishwa ili iweze kuendana. Hii ni kuhakikisha kwamba mfumo wa elimu unazalisha au kuandaa aina ya raia wanaohitajiwa au watarajiwao na nchi. Pia, mtaala huu unazingatia hoja kuwa kuna mambo mengi yanayoathiri kitu ambacho watoto wanafundishwa, ni kwa namna gani wanajifunza ipasavyo na ujuzi waupatao. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na mtaala sahihi, ubora wa walimu na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo. Hivyo basi, mtaala huu umeyazingatia vilivyo mambo haya ili kuhakikisha ubora wa elimu .Nia ya kujenga jamii yenye kuegemea katika maarifa na kukua kwa ushindani wa kikanda na kiulimwengu katika soko la ajira, imelazimisha au kuchangia kuhamia katika mtaala uegemeao katika ujuzi. Hivyo basi, wanafunzi wakisaidiwa na walimu wao ambao kwa hakika wana wajibu muhimu katika kuhakikisha kuwa muhtasari huu unafanikiwa wanapata stadi na ujuzi sahihi na pia waweze kuyatumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wataonesha tofauti sio tu katika maisha yao bali pia kwa ustawi wa taifa. Ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa watu wote waliochangia katika uandaaji wa nyaraka hii, hususani REB na wafanyakazi wote walioandaa na kusimamia mchakato wote kuanzia pale ulipoanzia kufika mwisho. Pia shukrani za dhati kwa wabia wetu wa kimaendeleo waliofadhili zoezi hili kwa kipindi chote.

Tunawaomba wale wote watakaotumia muhtsari huu kutoa maoni yatakayosaidia uboreshaji wake

**GASANA I. Janvier**

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Elimu Rwanda

**SHUKRANI**

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa watu wote walioshiriki kwa hali na mali katika kutengeneza na kufanikisha muhtasari huu. Muhtasari huu usingeweza kufanikiwa bila kuwepo wadau mbalimbali katika Nyanja za elimu walioshiriki kwa hali na mali katika kuugharimia na kuuandika .

Shukrani zangu za dhati ziwaendee Taasisi na watu watu walioshiriki kama ifuatavyo :

Bodi ya Elimu Rwanda na wafanyakazi wake wote walioshiriki katika uandaaji na uandishi wa muhtasari huu, walimu wote toka chekechea, sekondari hadi chuo kikuu waliochangia katika ufanikishaji wa muhtasari huu.

Shukrani pia zizidi kuwaendea wadau mbalimbali wa Elimu kama: UNICEF,UNFPA pamoja na Aceess to Finance Rwanda kwa kugharimia na kufanikisha shughuli hii .

Tutazidi kushukuru na kuthamini mchango wa mashirika mbalimbali ya Elimu kama

CNLG, AEGIS trust, Itorero ry'Igihugu, Gender Monitoring Office, National Unit and Reconciliation Commission, RBS, REMA, Handicap International, Wellspring Foundation, Right To Play, MEDISAR, EDC/L3, EDC/Akazi Kanoze, Save the Children, Faith Based Organisations, WDA, MINECOFIN and Local and International consultants

Msaada wao, ushirikiano wao na ujuzi wao vimekuwa changamoto katika kufanikisha upatikanaji wa muhtasari mpya katika idara ya Mitaala, Mbinu za Ufundishaji na Utengenezaji wa Vifaa vya ufundishaji (CPMD).

**Dr. MUSABE Joyce ,**

Naibu Mkurugenzi Mkuu CPMD; Mitaala, Mbinu za Ufundishaji na Utengenezaji wa Vifaa vya ufundishaji.

**WALIOSHIRIKI KATIKA KUTUNGA MUHTASARI HUU**:

**Bodi ya Elimu Rwanda**

- Dr MUSABE Joyce : Naibu Mkurugenzi Mkuu wa CPMD: Mitaala, Mbinu za Ufundishaji na Utengenezaji wa Vifaa vya ufundishaji
- GATERA Augustin: Mkurugenzi wa Kitengo cha Lugha na Sayansi za Jamii
- RUBAYA Anthony: Mkuu wa Kitengo cha Ukuzaji Mitaala Somo la Kiswahili

**Walimu na wahadhiri**

- WALLACE Mlaga: Chuo Kikuu cha Rwanda, Koleji ya Elimu
- RUZINDAZA Bonaventure:Ecole Secondaire Saint Joseph le Travailleur (ESSJT).
- MUZUNGU Innocent: Ecole Secondaire Rurama
- MUPENZI Theodore: Kagarama Secondary School
- NSHOGOZA Jean Damascene: Groupe Scolaire Ndera.

**Mhariri**

Dr NIYOMUGABO Cyprien:Chuo Kikuu cha Rwanda, Koleji ya Elimu

**Washiriki wengine**

-Dr RWANAMIZA Erasmus AEGIS trust

YALIY0MO

DIBAJI ..... i
SHUKRANI..... ii
WALIOSHIRIKI KATIKA KUTUNGA MUHTASARI HUU: ..... iii
YALIY0MO..... iv
1. UTANGULIZI ..... 1
1.1. Usuli wa mapitio ya mtaala ..... 1
1.2. Sababu ya kufundisha na kujifunza Kiswahili nchini Rwanda ..... 1
1.2.1. Kiswahili na jamii..... 2
1.2.2. Kiswahili na mwanafunzi..... 3
1.2.3. Ujuzi..... 3
2. MKABALA WA UFUNDISHAJI ..... 7
2.1. Majukumu ya mwalimu ..... 7
2.2. Majukumu ya Mwanafunzi ..... 8
2.3. Mikakati ya kukabiliana na mahitaji maalumu ya kielimu ..... 9
3. MKABALA WA TATHMINI..... 10
3.1. Aina za tathmini..... 10
3.1.1. Tathmini endelezi ifanyikeyo shuleni ( Tathmini ye kuyifunza) ..... 10
3.1.2. Upimaji wa jumla (Upimaji wa kujifunza) ..... 11
3.2. Utunzaji wa alama ..... 12
3.3. Vigezo katika kuandika upimaji wa kiujumlishaji..... 12
3.4. Ripoti kwa wazazi..... 13
4. ZANA AU VIFAA ..... 14
4.1. Zana na mikakati ya ufundishaji ..... 14
4.2. Orodha ya vifaa au zana zinazohitajika katika ufundishaji ..... 14

5. MADA NA SURA ZA UFUNDISHAJI ..... 15
5.1. Muundo wa muhtasari ..... 15
5.2. Kidato cha nne ..... 16
5.2.1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha nne ..... 16
5.2.2 Muhtasari wa kidato cha nne ..... 17
5.3. Kidato cha tano ..... 27
5.3.1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha tano ..... 27
5.3.2. Muhtasari wa kidato cha tano ..... 28
5.4. Kidato cha sita ..... 38
5.4. 1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha sita ..... 38
5.4.2. Muhtasari wa kidato cha sita ..... 39
6. MAREJEO ..... 47
7. VIAMBATANISHO: ..... 48

# 1. UTANGULIZI

## 1.1. Usuli wa mapitio ya mtaala

Muhtasari huu mpya wa Kiswahili wa kidato 4-6 utatumiwa badala ya ule wa mwaka 2010. Hii ni kutokana na haja ya kuzingatia zaidi mahitaji ya mwanafunzi na kumfanya awe na maarifa, ujuzi na uwezo wa kuyaweka katika vitendo yale aliyojifunza katika mazingira mbalimbali ya kimaisha atakayokumbana nayo. Hii ni tofauti na muhtasari wa awali uliokuwa umeegemea katika madhumuni ya kumfanya mwanafunzi awe na maarifa tu. Hivyo basi, muhtasari huu umeweka msisitizo katika kujenga zaidi stadi na ujuzi kuendana na maudhui yaliyokuwepo katika muhtasari wa awali. Hii ina maana kwamba mtaala huu ni ule uegemeao katika ujuzi kama inavyobainishwa katika mpango mkakati wa sekta ya Elimu 2013/14- 2017/2018 (ESSP). Pia, kuna mabadiliko kadhaa ya kimaudhui yaliyofanyika ili kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kujikita zaidi katika kuwawezesha wanafunzi kuzimudu vema stadi za lugha ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika.

Muhtasari huu mpya wa Kiswahili unatoa mwongozo wa maingiliano kati ya mwanafunzi na mwalimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji huku ukibainisha stadi za kivitendo na ujuzi ambao mwanafunzi ataupata wakati anapojifunza na baada ya kufika mwisho wa kila sura au mada ya ujifunzaji.

## 1.2. Sababu ya kufundisha na kujifunza Kiswahili nchini Rwanda

Kiswahili ni lugha ya Afrika inayoongelewa na watu wengi barani Afrika na Ulimwenguni kwa ujumla. Jamii ya Rwanda imezungukwa na nchi ambazo zinazungumza Kiswahili. Kwa maana hii, tunahitaji kuwasiliana nao katika nyanja mbalimbali kama kisiasa , kiuchumi na kijamii kwa sababu ni lugha inayoongelewa katika nchi wanachama wa jumuia ya Afrika ya Mashariki ambapo Rwanda ni mwanachama.

### 1.2.1. Kiswahili na jamii

Lugha ni nyenzo muhimu katika maisha ya binadamu na jamii kwa ujumla kwani humwezesha mtu kufanya mawasiliano kwa madhumuni mbalimbali. Kwa kutumia lugha, binadamu au jamii huwa na fursa ya kuweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Lugha huweza pia kuunganisha jamii au jamii na jamii. Kwa namna nyingine, inaweza kubainishwa kuwa lugha ni msingi wa maendeleo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kupitia lugha shughuli mbalimbali za kimaendeleo huchochewa. Lugha pia ni nyenzo muhimu katika kudumisha amani katika jamii yoyote. Hivyo basi, lugha ni nyenzo muhimu kabisa inayopaswa kupewa kipaumbele katika jamii yoyote.

Nchini Rwanda kuna lugha nyingine kama vile Kinyarwanda, Kiingereza, na Kifaransa ambazo zinafundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu na kwa malengo mbalimbali. Tofauti hizi za malengo au sababu za ufundishaji wa lugha hizi ndio msingi wa kuona umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika kuifundisha na kujifunza nchini Rwanda. Sababu ya msingi ya kufundisha lugha ya Kiswahili ni nafasi ya lugha hiyo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Kiswahili kimepewa nafasi kubwa kwa nchi nyingine washiriki wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuwa Rwanda ina ushirikiano na nchi hizi kama vile ushirikiano wa kijamii, kibiashara, na kiutamaduni, lugha ya Kiswahili haiepukiki katika kufanikisha vema ushirikiano huu kuliko lugha nyingine yoyote hususani katika mawasiliano yanayojumuisha jamii pana. Pia inaelezwa kuwa mojawapo ya mashariti ya Rwanda kukubaliwa kujiunga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikuwa ni pamoja na kukubali kutumia lugha ya Kiswahili (Kawoya, 2009:7). Mkuthuria, (2006) anaeleza kuwa kifungu cha 19 (d) cha mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kinasisitiza suala la ukuzaji na uendelezaji wa lugha za kiasili hususani lugha ya Kiswahili kama lugha mawasiliano ya ukanda (Lingua Franca). Hii ina maana kwamba wakati Rwanda ilipokusudia kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tayari ilikuwa inajua umuhimu na nafasi ya Kiswahili kama lugha mawasiliano katika ukanda huu. Hivyo basi, mazingira hayo yote yaliyobainishwa ndio msingi mkuu wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda.

### 1.2.2. Kiswahili na wanafunzi

Kiswahili ni somo muhimu katika maisha ya wanafunzi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba licha ya umuhimu wake katika mawasiliano kwa jumla, Kiswahili kinahitajika katika baadhi ya taaluma au ajira ambazo mwanafunzi anaweza kuingia. Taaluma au ajira hizi ni pamoja na uandishi wa habari, biashara, huduma kwa wateja, uongozaji watalii, ukalimani na tafsiri. Hivyo, somo la Kiswahili linamwezesha mwanafunzi kumudu ipasavyo stadi zote nne za mawasiliano ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa ufasaha katika miktadha tofauti anayoweza kukutana nayo katika maisha yake ya kila siku. Pia, wanafunzi wanapata fursa ya kupata stadi za kushiriki kwa ufasaha katika mawasiliano rasmi na yasiyo rasmi. Hii inawasaidia wanafunzi kwa sasa na baadaye katika kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi, na kisiasa ambazo zinahitaji matumizi ya lugha ya Kiswahili ili kuzifanikisha kwa ukamilifu. Hii ni kwenda sambamba na Progaramu ya Serikali ya Miaka Saba (7YP) 2010 – 2017.

### 1.2.3. Ujuzi

Ujuzi wa msingi umeoyeshwa kama ilivyotajwa katika upana wa ujuzi wa somo na kujitokeza katika malengo yaliyoonyeshwa mwaka hadi mwaka kuhusiana na mada zinazofundishwa.

Uchaguzi wa aina za ufundishaji lazima ulenge kuhusu ujuzi ambao mwanafunzi ataweza kuuonyesha wakati wowote wa kujifunza hadi atakapohitimu.

Ujuzi wa msingi ambao utasisitizwa na kuonyeshwa katika mchakato wa ujifunzaji, umeelezewa kwa ufupi katika aya za chini na mwalimu atahakikisha kuwa wanafunzi watahawalisha majukumu ambayo yatawasaidia kupata stadi hizo.

**Tafakari na utatuzi wa matatizo ya stadi:** Upatikanaji wa stadi hizi utamsaidia mwanafunzi kufikiri kwa mapana kutathmini na kutafuta suluhisho kwa matatizo atakayokumbana nayo katika mazingira yoyote.

**Ubunifu na ugunduzi:** Upatikanaji wa stadi hizi utamsaidia mwanafunzi kuamua na kufikiri zaidi ya mawanda ya ufahamu kwa kutoa mawazo mapya na kujenga dhana mpya.

**Utafiti**i**:** Hii itawasaidia wanafunzi kutafuta majibu ya maswali ya msingi kuhusiana na habari na dhana zilizopo na kuelezea hali kuhusiana na utafiti kutoka habari liyopatikana.

**Mawasiliano katia lugha rasmi:** Walimu watahakikisha matumizi bora ya lugha na maelekezo kwa wanafunzi ambayo yatawasaidia kuwasiliana vizuri na kutoa mawazo mwafaka kwa kusema, kuandika na kutumia sarufi sahihi ya lugha na msamiati husika.

**Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha:** Hii itamsaidia mwanafunzi kushirikiana na wenzake katika kundi katika kazi yoyote atakayopewa, kuwa na mwelekeo chanya na maadili, kuheshimu haki na maoni ya wengine na kufanya shughuli zihusianazo na kuhifadhi na kutunza mazingira.

**Ujifunzaji wa muda mrefu :**Upatikanaji wa stadi hizi utawasaidia wanafunzi kupata maarifa na stadi kwa kiwango kinachoweza kuendana na mabadiliko ya maarifa ya kiwango cha juu cha mahitaji binafsi katika maeneo ambayo yanahitaji marekebisho na maendeleo. Kujifunza kiswahili huimarisha na kupanua akili na ni muhimu kwa uendelezaji wa tafakuri tunduizi na hasa tafakari, upimaji na ubinifu. Kwa kusoma vitabu, wanafunzi wataweza kugundua hali za binadamu na kuzama katika uelewa wao kuhusu utamaduni na maadili, masuala ya kijamii katika jamii zao na kutoka tamaduni zingine ulimwenguni kwani wanafunzi huvutwa na usasa na ukale.

Mada kuhusu maisha yao na dunia waishimo kwa kiwango cha stadi za kufikiri kwa kusoma vitabu na kujifunza lugha itawasaidia kujifunza na kutumia waliyojifunza katika hali halisi.

Mawanda kukuza lugha ya Kiswahili

Katika mchakato wa ujifunzaji, mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kufanya mawasiliano na watu kutoka katika nchi zinazozungumza Kiswahili.
- Kujieleza kwa kutumia Kiswahili kwa njia ya mazungumzo na kuandika huku akitumia msamiati sahihi na sarufi sahihi inayoendana na kiwango chao cha ujifunzaji na kwa kuzingatia mawasiliano ya kila siku.
- Kusikiliza na kutafsiri taarifa za Kiswahili kwa usahihi.
- Kusoma kwa kujiamini na kuelewa aina mbalimbali za matini za kifasihi na zisizo za kifasihi.
- Kutoa taarifa, mawazo, hisia kwa usahihi na ufasaha katika miktadha mbalimbali ya kijamii na kiutamaduni.
- Kutumia Kiswahili kwa ufasaha anaposhiriki katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali nchini Rwanda hususani zile zinazohitaji matumizi ya lugha ya Kiswahili.
- Kuonesha umilisi mzuri wa msamiati na ruwaza ya lugha ya Kiswahili katika mazungumzo na maandishi
- Kufanya uhakiki wa kazi yoyote ya kifasihi katika matini andishi au simulizi.

Kiswahili na ukuzaji wa ujuzi

Nyaraka kuhusu sera ya taifa inayoegemezwa katika matarajio ya taifa inabainisha baaadhi ya ujuzi wa msingi pamoja na ujuzi wa jumla kama inavyobainishwa katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Awamu ya Pili (EDPRS 2), Sera ya Sekta ya Elimu (ESP) na katika Mpango Mkakati wa Sekta ya Elimu (ESSP). Ujuzi huu ndio utarajiwao kukuza au kufanikisha ujuzi wa kiwango

cha juu cha kufikiri. Pia, ujuzi huu ndio utakaosaidia ujifunzaji wa somo na kuweza kuyatumia yale yaliyofundishwa au kujifunza katika mazingira halisi ya kimaisha.

Katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili, ujuzi wa jumla unapewa kipaumbele sana. Ujuzi huu wa jumla ni pamoja na tafakuri tunduizi, ubunifu, utafiti na utatuzi wa matatizo na ushirikiano. Haya yote yanafanikishwa kwa kuhakikisha kuwa mwanafunzi hususani mahitaji yake ndilo linakuwa ni jambo la msingi katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Wanafunzi watapewa kazi mbalimbali zinazohitaji washirikiane ili kukamilisha, kufanya tafiti au kutatua changamoto mbalimbali katika maisha kupitia midahalo na majadiliano mbalimbali. Kila ufundishaji na ujifunzaji kwa kila somo lililoandaliwa linazingatia nafasi ya kumjengea mwanafunzi stadi sahihi za mawasiliano katika miktadha mbalimbali ya kimaisha. Pia, ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili unatoa nafasi ya kuhakikisha kuwa ujuzi wa msingi unajengwa miongoni mwa wanafunzi. Ujuzi huu ni kama vile  kusoma na kuandika, kuhesabu, mawasiliano katika lugha ya kigeni ambayo ni Kiswahili, sayansi na teknolojia, ujuzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA), stadi ya menejimenti ya mtu binafsi na mahusiano na watu wengine na zile za maisha, uraia na utambulisho wa kitaifa, ujasiriamali na uanzishaji wa biashara na ujifunzaji usio na kikomo. Haya yote yanafanikishwa kwa namna ambavyo Kiswahili kinafundishwa na namna wanafunzi wanavyojifunza Kiswahili. Mada mbalimbali zinazojenga muktadha wa kujifunza lugha ni zile zinazokuza ujuzi wa msingi kwa mwanafunzi. Pia, sayansi na teknolojia au ujuzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano inatumika katika kujifunza lugha ya Kiswahili ili kuendana na Mwelekeo wa Rwanda hadi kufikia mwaka 2020 (Vision 2020).

## 2. MKABALA WA UFUNDISHAJI

Wanafunzi hujifunza vizuri zaidi pale wanaposhirikishwa kama watendaji katika mchakato wa ujifunzaji. Hii inawezekana pale wanafunzi wanapowezeshwa kuwa na kiwango cha juu sana cha ushiriki, michango, na hata ufanikishaji wa somo husika. Wakati huo huo ni muhimu kutambua kuwa kila mwanafunzi mmoja mmoja ni mtu mwenye mahitaji binafsi, kasi ya ujifunzaji, tajiriba (uzoefu) na uwezo. Hivyo basi, ni muhimu mikakati ya ufundishaji iwe ya aina tofauti na yenye uwezekano wa kubadilika ili kuendana na mahitaji ya wanafunzi na aina ya mada inayofundishwa katika somo linalofundishwa. Pamoja na hayo, mbinu ya kuegemea kwa mwanafunzi katika elimu isichukuliwe kwa maana ya kwamba sasa mwalimu hana wajibu wowote katika kuhakikisha ujifunzaji unaofanikiwa ipasavyo.

### 2.1. Majukumu ya mwalimu

Mabadiliko ya kuelekea katika mtaala unaoegemea katika ujuzi yanahusu mabadiliko ya ujifunzaji, yaani kuhakikisha kuwa ujifunzaji unakuwa ni wa kina, wa kuvutia na wenye ujenzi wa tabia. Walimu wanajikuta wakihama kutoka katika mbinu ya zamani ya utoaji maarifa na badala yake wanajikuta wakiwa na wajibu wa kuwa wawezeshaji ili kuhakikisha matarijio na mahitaji binafsi ya wanafunzi yakipewa kipaumbele au kuzingatiwa. Kutokana na hali hii, mwalimu anawajibika kubainisha mahitaji ya wanafunzi, namna ujifunzaji utakavyofanyika na namna ya kuongoza tajiriba ya ujifunzaji ipasavyo.

Wajibu wa mwalimu ni kuwaongoza wanafunzi ndani ya darasa na nje ya darasa kushiriki kupitia mbinu mbalimbali shirikishi kupitia mchakato wa ujifunzaji kama mwanafunzi mmoja, katika jozi au katika makundi. Hii inahakikisha kuwa ujifunzaji unatawaliwa na utendaji wa watu, unakuwa hai na shirikishi, na wenye kuzingatia ushirikiano. Mwalimu atabuni na kuwapatia wanafunzi kazi mbalimbali za kufanya au kwa ajili ya majadiliano ya papo kwa papo. Hii ina maana kwamba wajibu wa mwalimu itakuwa ni kutoa mwongozo kwa wanafunzi katika kujenga maarifa yao wenyewe kuliko kuwapatia maarifa.

Wanafunzi wanafundishwa namna ya kutumia vitabu vya ziada na kiada katika namna mbalimbali. Inaweza kuwa kutafiti au kutafuta taarifa na kuzitumia katika kujiandalia notisi zao wenyewe. Hii ni tofauti na mwalimu kuwaandalia wanafunzi notisi.

Mwalimu ni lazima achague kuandaa zana mwafaka za ufundishaji. Zana hizi ni pamoja na modeli za ufundishaji, chati za kutumiwa na wanafunzi katika kazi zao. Mwalimu ni lazima atoe mfano wa namna ya kusoma au kutamka baadhi ya maneno kabla wanafunzi nao hawajafuatisha. Baada ya mwongozo huo ni muhimu wanafunzi wapewe nafasi ya kutosha katika ujifunzaji. Pia, ni muhimu kwa mwalimu kuandaa mikakati ya kuwawezesha wanafunzi kuendelea kujifunza au kukitumia kile walichojifunza darasani hasa wanapokuwa nje ya darasa. Ni wajibu tena wa mwalimu kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kufanikisha kujifunza somo lililokusudiwa kwa ufanisi.

## 2.2. Majukumu ya Mwanafunzi

Kazi zinazopaswa kufanywa na mwanafunzi zimeoneshwa kwa kila sura. Kazi hizi zinaakisi ushirikishwaji muafaka wa mwanafunzi katika mchakato wa ujifunzaji. Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji utaongozwa na kusudio la kujenga mazingira rafiki ya mwanafunzi kwa kuzingatia uwezo, mahitaji, uzoefu na mapendeleo. Pia, kazi au shughuli za ujifunzaji zitapangiliwa katika namna ambayo itahamasisha wanafunzi kujenga maarifa kama mtu mmoja mmoja au katika makundi kwa ushiriki ulio hai. Wanafunzi watafanyia kazi ujuzi mmoja kwa wakati mmoja katika muundo wa sura zenye malengo mahsusi ya ujifunzaji yaliyogawanyika katika maarifa, stadi na mwenendo mwema. Katika baadhi ya kazi za ujifunzaji watafanya katika vikundi ili kujenga muktadha sahihi wa kimawasiliano

### 2.3. Mikakati ya kukabiliana na mahitaji maalumu ya kielimu

Kila Munyarwanda anayo haki ya kupata elimu bila kujali tofauti za mahitaji zilizopo. Msingi wa yote haya ni kuonyesha kuwa raia wote wanafaidika kutokana na mpago wa elimu uliopo. Uwezekano wa fikra hii ni kulenga hasa katika mahitaji ya elimu. Ugumu wa haya ni kwamba tunao raia /wanafunzi ambao wanaotofautiana katika hali zao kimaisha na wengi wasiopendelea elimu. Tofauti zaweza kuwa hisia, mabavu, Nyanja za fahamu zinazolenga katika mgongano wa elimu ya ukale zinazojulikana kama utahira.

Wanafunzi wote hawa wana haki sawa ya kufaidi kutokana na mfumo wa msingi wa lazima wa elimu wa kila siku katika sehemu zao. Kwa maana hii, majukumu ya shule ni kuwaorodhesha na kupanga mikakati ya kumpa kila mtu kulingana na elimu inayomfaa katika mchakato wa kusoma na kujifunza.

Mikakati ya tathmini na hali itabidi iwe kaika ukokotoaji wa mahitaji ya wanafunzi hawa. Ushauri wa kila kundi la wanafunzi wenye elimu maalumu utatolewa kulingana na ushauri wa walimu.

# 3. MKABALA WA TATHMINI

Tathmini ni mchakato wa kupima ufundishaji na ujifunzaji kwa kukusanya na kutafsiri vigezo binafsi vya mwanafunzi katika mchakato wa kujifunza na kuvitolea uamuzi kuhusu mafanikio ya mwanafunzi kuhusu upimaji wa viwango vilivyotolewa. Tathmini ni sehemu muhimu katika mchakato wa kujifunza. Katika mtaala wa upimaji wa ujuzi tathmini inapaswa iwe imelenga katika ujuzi ambao mwanafunzi atapewa,mazingira mchanganyiko au magumu yanayohusiana na maisha yake ya kila siku na kuambiwa atumie aliyojifunza katika kupampana au kujitatulia matatizo hayo.

Tathmini itapangwa au kufanywa katika ngazi zifuatazo: Tathmini katika ngazi za shule; mitihani ya wilaya; tathmni ya kitaifa (LARS) na mtihani wa taifa.

## 3.1. Aina za tathmini

### 3.1.1. Tathmini endelezi ifanyikeyo shuleni ( Tathmini ye kuyifunza)

Tathmini endelezi inatumia mbinu rasmi na zisizo rasmi zitumikazo shuleni kuangalia kama ujifunzaji unafanyika kama inavyokusudiwa au la. Wakati mwalimu anapoandaa somo lake anapaswa kuonyesha vigezo vya ufaulu na mabadiliko ya mwenendo anapoanza kufundisha sura mpya. Baada ya kumaliza kila mada ,mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wamemudu yaliyoongelewa katika ujuzi upatikanao katika kila mada kabla ya kuanza kujifunza mada inayofuata. Mwalimu atapima jinsi kila mwanafunzi atakavyomudu vizuri somo lake pamoja na tafakuri tunduizi zilizoelezwa katika muhtasari. Kutokana na haya mwalimu atapata picha halisi kuhusu maendeleo ya ujifunzaji wa wanafunzi.

Mwalimu atatumia moja au mchakato wa yafuatayo (a) Utafiti (b) Kalamu na Karatasi (c) Maswali dodoso au majaribio ya kuzungumza.

### 3.1.2. Upimaji wa jumla (Upimaji wa kujifunza)

Wakati upimaji unapotumiwa kurekodi ujuzi uliopatikana katika ujifunzaji wa mwanafunzi, inakuwa inalenga upimaji wa jumla. Upimaji wa jumla hutoa picha ya ujuzi au mwelekeo maalum kwa muda fulani.

Makusudi muhimu ya upimaji wa jumla ni kutathmini kuwa malengo ya kujifunza yamefikiwa na kutumia matokeo ya kurekodi au ngazi ya mwanafunzi, kwa kutoa uamuzi wa maendeleo yake, kwa kuchaguliwa katika ngazi nyingine ya elimu au ngazi ya kupata cheti.

Tathmini hii ni lazima iweke pamoja mwelekeo au maoni ambapo mwanafunzi ataweza kuonyesha alivyomudu ujuzi wote alioupata katika ujifunzaji.

Inaweza ikawa upimaji shuleni au nje ya shule kwa muundo wa mitihani wa taifa. Upimaji wa jumla shuleni hususani ule wa kila mtihani wa somo unapaswa kufanyika mara moja mwishoni mwa kila muhula wa masomo na mara moja tena mwishoni mwa kila mwaka wa masomo. Wastani wa matokeo ya upimaji wa jumla shuleni kwa kila somo utapimwa, kurekodiwa na kuwekwa miongoni mwa matokeo ya mtihani wa mwisho wa kitaifa .

Wastani wa upimaji wa jumla shuleni utachangia asilimia fulani pindi walimu watakapopata uzoefu na kujiamini katika nyanja za upimaji na itakapofikia mwaka wa tatu katika utumiaji au uendelezaji wa mtaala mpya, wastani utachangia asilimia kumi (10%) katika mtihani wa mwisho, hii itaenda hatua kwa hatua .

Wilaya zitahamasishwa au kuungwa mkono kuendeleza ubunifu na kupanga mitihani ya kawaida kwa madarasa kwenye shule zote kwa kutathmnini matokeo na mafanikio ya wanafunzi katika kila shule. Upimaji nje ya darasa utafanyika mwishoni mwa kidato cha tatu na cha sita.

### 3.2. Utunzaji wa alama

Huu ni ukusanyaji wa vigezo vya ukweli na vidhibiti kutoka vyombo vya upimaji na kuvitumia katika kutolea hukumu kuhusu ufaulu wa mwanafunzi kwa kuonyesha vigezo vilivyowekwa. Vigezo vyovyote vya tathmini vitakavyotumiwa vitatoa data katika muundo wa matokeo ambao utarikodiwa na kuhifadhiwa vizuri katika faili kwa sababu zitachangia katika maendeleo ya mwanafunzi na itakuwa kumbukumbu kwa mwanafunzi pamoja na wazazi kwa kuangalia maendeleo ya ujifunzaji wake na kumpa ushauri kulingana na mtihani wa mwisho wa wanafunzi .

Jarada ni faili(au data zilizokwekwa kwenye kompyuta) zikiwa na kazi za mwanafunzi pamoja na tathmini zake zikionyesha jitihada na udhaifu wa kazi. Jarada halionyeshi kazi zilizofanyika pekee yake (kama karatasi na majaribio)bali ina rekodi za mazoezi yaliyofanyika kwa muda mrefu kama sehemu ya ujifunzaji wa mwanafunzi.Mapato au matokeo (upimaji wa jumla) yatafikiriwa pekee kama yametosha kwa miaka mitatu ya kidato cha nne tano na sita. Zaidi ya hayo yatakuwa kama vigezo vya sifa kwa kila mwanafunzi aliyehudhuria mfumo wote wa ujifunzaji kabla ya kuingia upimaji wa ujumlishaji kwa kila somo.

### 3.3. Vigezo katika kuandika upimaji wa kiujumlishaji

Kabla ya kuandaa karatasi ya maswali, mpango wa kile kitakachoulizwa lazima uandaliwe kwa kuonyesha sura au mada zitakazoulizwa, idadi ya maswali kwa kila kiwango cha Bloom`s taxonomy na kuonyesha alama zilizopangwa kwa kila swali. Katika mtihani upimao ujuzi, maswali kutoka katika kila kiwango cha Bloom`s taxonomy yanatakiwa yapewe uzito kuliko yale yatayotoka katika kiwango cha maarifa na ufahamu.

Kabla ya kuandaa karatasi ya maswali, mwandishi lazima ahakikishe jaribio au maswali ya mtihani lazima yapangwe sambamba na upimaji wa ujuzi kwa kufanya yafuatayo :

- Kutambua mada za kuuliza kutoka muhtsari kulingana na somo.
- Kufupisha yaliyomo katika somo ukifikiria kuwa ndio msingi wa zoezi.
- Kutambua matokeo ya kujifunza yatakayopimwa katika zoezi
- Kuandaa jedwali la mambo muhimu yanayotakiwa.

--Kuhakikisha kuwa vitenzi vilivyotumiwa katika uandaaji wa maswali havihitaji kumbukumbu kukumbuka pekee yake bali vinavyopima mawanda ya ujuzi kama ilivyoonyeshwa katika muhtasari.

**Muundo wa mtihani wa Kiswahili kidato cha 4-6 mchepuo wa lugha**

Baada ya mwisho wa masomo kutakuwapo na mitihani miwili kama ifuatavyo :

**<u>Mtihani wa kanza 1</u>**

Mtihani wa kwanza utakuwa nasehemu zifuatazo : Sehemu ya kwanza :**Ufahamu , Sarufi ,Utungaji**

**<u>Mtihani wa pili 2</u>**

Mtihani wa pili utakuwa na sehemu zifuatazo

**Sehemu ya A** : **Nadharia ya Fasihi**

**Sehemu B : Uhakiki wa tanzu za fasihi katika kiswahili**

**3.4. Ripoti kwa wazazi**

Uwanda wa kujifunza katika mtaala mpya ina maana kuwa ni lazima kufikiri namna ya kushirikisha wazazi katika ujifunzaji wa mwanafunzi. Utoaji wa maoni pekee hautoshi kulezea matarajio tofauti yaliyomo katika malengo ya kujifunza. Ripoti iliyo muhimu ni kushirikiana na wanafunzi kuhusu utendaji mzuri na kuangalia pale panapohitajiwa kufanyiwa marekebisho. Skeli muhimu ya kufikia malengo vizuri, matarajio ya mikutano na siyo malengo ya mikutano kwa kila maarifa na stadi za somo na ujuzi wa somo vitatoa ujumbe mwafaka kuliko maoni ya mtu mmoja. Kuhusu upimaji shuleni huu, siyo lazima alama zake zirekodiwe **.**4. ZANA AU VIFAA

# 4. ZANA AU VIFAA

## 4.1. Zana na mikakati ya ufundishaji

Sehemu hii inajadili mahitaji ya msingi yanayohitajika ili utekelezaji wa muhtasari huu uweze kufanyika kwa ufanisi mkubwa. Mahitaji haya ya msingi ni pamoja na orodha ya vifaa au zana zinazohitajika katika ufundishaji, ujuzi unaohitajika kwa mwalimu wa somo hili katika kiwango hiki, na mikakati ya kuzingatia katika kukabiliana na mahitaji maalumu katika elimu. Vipengele hivi vinafafanuliwa kama ifuatavyo katika sehemu inayofuata:

## 4.2. Orodha ya vifaa au zana zinazohitajika katika ufundishaji

Zana na vifaa vilivyopendekezwa kwa kila mada au sura zinaweza kutumika katika kufundishia pamoja na nyingine ambazo mwalimu ataona zinafaa kutokana na mazingira yake. Mwalimu anashauriwa kuwa mbunifu, kutumia na kutafuta zana mbadala kulingana na upatikanaji wa vifaa hivyo katika mazingira yake. Baadhi ya vifaa ambavyo vinaweza kutumika mara kwa mara ni pamoja na redio, picha za vifaa na vitu mbalimbali katika mazingira mbalimbali, picha za watu wa rika mbalimbali wakiwa katika miktadha tofauti, simu ya mkononi, kanda za sauti zenye mazungumzo na hotuba za Kiswahili, vitabu, matini au vifungu mbalimbali vya mazungumzo.

# 5. MADA NA SURA ZA UFUNDISHAJI

## 5.1. Muundo wa muhtasari

Muhtasari huu una sehemu kuu nane ambazo ni utangulizi, malengo ya jumla mwishoni mwa kila kiwango, mikabala ya mbinu za ufundishaji, mikabala ya upimaji, vifaa vya ufundishaji, sura za muhtasari, marejeleo na viambatanisho. Sehemu hizi ni utangulizi na sura za muhtasari. Vipengele vinavyojitokeza katika utangulizi ni pamoja na usuli, sababu za ufundishaji Kiswahili nchini Rwanda, ujuzi wa jumla na mwenendo mwema utarajiwao kwa wanafunzi.

Kila sura ya muhtasari imeundwa na jedwali. Jedwali hili lina safu tano zinazohusika na ufundishaji na ujifunzaji wa sura au mada inayobainishwa katika jedwali husika. Safu ya kwanza inahusika na maarifa na ufahamu. Kiwango hiki kinahusu ushughulishaji wa akili ya mwanafunzi katika kiwango cha chini cha kazi kama kurudia, kueleza, kutaja, kuonesha n.k. Hiki ni kiwango cha chini cha fikra kwa mujibu wa ufafanuzi wa Bloom. Safu ya pili inahusika ni kiwango cha juu sana cha fikra kwa mujibu wa ufafanuzi wa Bloom. Kiwango hiki kinahusu ushughulishaji wa akili ya mwanafunzi katika kiwango cha juu cha kazi kama uchambuzi, ufafanuzi, kufanya muhtasari, kutathmini, kutumia mifano n.k. Safu ya tatu inahusika na maadili na mwenendo mwema unaokusudiwa kujengwa kwa mwanafunzi kupitia mada au sura inayofundishwa. Safu ya nne inahusu yaliyomo. Haya ni maudhui ya msingi yanayokusudiwa kufundishwa katika mada au sura husika ili kufikia malengo ya kimaarifa na ufahamu, stadi na hata mwenendo mwema. Safu ya tano inahusu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji. Mbinu hizi zimeegemezwa katika kazi atakazozifanya mwanafunzi ili kukamilisha mchakato wa ujifunzaji. Jedwali hili pia lina safu mlalo zilizopangwa ifuatavyo: Uhusiano wa mada husika na mada au sura nyingine katika masomo mengineyo, vigezo vya tathmini au upimaji, na zana au vifaa vya ufundishaji wa sura au mada husika.

Muhtasari huu wa kidato cha nne hadi cha sita una jumla sura/mada 13; kidato cha nne kina jumla ya mada au sura tano; kidato cha tano sura nne; kidato cha sita sura nne

| | Kidato cha 4 | Kidato cha 5 | Kidato cha 6 |
|---|---|---|---|
| Mada kuu | 5 | 4 | 3 |
| Mada ndogo | 5 | 4 | 4 |
| sura | 5 | 4 | 4 |

### 5.2. Kidato cha nne

#### 5.2.1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha nne

Inatazamiwa kwamba mwanafunzi amalizapo kidato cha nne ataweza:

- Kuwasiliana kwa mazungumzo na maandishi na watu au jamii katika miktadha mbalimbali.
- Kuandika aina mbalimbali za insha za kimasimulizi.
- Kuelewa na kuelezea dhima ya lugha katika jamii.
- Kueleza asili, kukua, na kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki.
- Kusoma na kuhakiki kazi za fasihi simulizi hususani utanzu wa hadithi.
- Kuainisha na kubainisha tanzu za fasihi ya Kiswahili na kueleza dhima ya fasihi katika jamii.
- Kusoma na kuelewa maandiko na vitabu mbalimbali vya Kiswahili vyenye taarifa ndefu ili kupata ujumbe uliomo.
- Kusikiliza na kuelewa kwa kina taarifa au habari mbalimbali kutokana na vyanzo vya habari zinazohusu masuala ya jamii.
- Kubaini matumizi sahihi ya maneno katika tungo mbalimbali za Kiswahili

### 5.2.2 Muhtasari wa kidato cha nne

| MADA KUU | MADA NDOGO | | | |
|---|---|---|---|---|
| **i.LUGHA NA JAMII** | **LUGHA YA KISWAHILI** | | **Idadi ya vipindi: 51** | |
| **Ujuzi upatikanao katika mada:** Kusikiliza, kusoma, kuzungumza na kuandika kwa minajili ya kuelewa lugha na umuhimu wake kama chombo cha mawasiliano katika jamii. | | | | |
| **Malengo ya kujifunza** | | | **Yaliyomo** | |
| **Maarifa na ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia** |
| – Kufafanua maana ya lugha kama chombo cha mawasiliano.<br><br>– Kuelezea umuhimu wa lugha katika jamii.<br><br>– Kuelezea asili ya lugha ya Kiswahili na chimbuko lake barani Afrika.<br><br>– Kukumbuka matumizi ya hali ya masharti kwa kutumia | – Kuonesha kimazungumzo na kimaandishi maana ya lugha.<br><br>– Kulinganisha umuhimu wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine katika mawasiliano ya kila siku katika jamii ya Wanyarwanda.<br><br>– Kuonesha njia ya ueneaji wa lugha ya Kiswahili toka pwani | – Kujivunia Kiswahili kama lugha yenye asili ya kiafrika.<br><br>– Kuimarisha desturi na umoja wa raia wa bara la Afrika kwa ujumla na raia wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa upekee kwa kutumia Kiswahili kama lugha ya | – Vifungu vya habari pamoja na maswali ya ufahamu kuelezea maana ya lugha.<br><br>– Vifungu vya habari pamoja na maswali ya ufahamu kuelezea lugha kama chombo cha mawasiliano.<br><br>– Vifungu vya habari pamoja na maswali ya ufahamu kuelezea kuenea kwa lugha ya Kiswahili toka pwani hadi Afrika ya Mashariki. | – Katika makundi, wanafunzi watajadili juu ya :<br>- Umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.<br>- Faida na hasara ya kutumia lugha moja ndani ya nchi (mfano wa Kinyarwanda)<br>- Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda.<br><br>– Wanafunzi watatunga visa vifupi ambavyo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| viambishi –nge-, -ngeli- au –ngali-. | hadi Rwanda.<br>– Kutunga sentensi tofauti au kusimulia juu ya kisa fulani kwa kutumia hali ya masharti. | mawasiliano. | – Sarufi: Matumizi ya viambishi vyenye dhana ya masharti -nge-, -ngeli- na -ngali-. | ndani yake watatumia hali ya masharti. |
| **Uhusiano wake na masomo mengine:** *Masomo ya historia, isimu, sosiolojia na mengineyo yanayohusika na mila na desturi za jamii.* | | | | |
| *Vigezo vya tathmini au upimaji: Uwezo wa kuelezea kwa ufasaha na kwa undani jinsi Kiswahili kilivyozaliwa na kuenea sehemu mbalimbali.* | | | | |
| *Zana au vifaa: Vitabu, mitandao ya intaneti, majarida, ramani ya Afrika yenye ukanda wa mashariki , bahari ya hindi na visiwa vilivyoko kwenye ukanda huu.* | | | | |

| MADA KUU | MADA NDOGO | |
|---|---|---|
| ii.LUGHA KATIKA SANAA | FASIHI KATIKA KISWAHILI | Idadi ya vipindi: 51 |

**Ujuzi upatikanao katika mada:** Kuelewa fasihi katika Kiswahili kwa ujumla kama sanaa inayoshughulikia jamii kwa kurahisisha mawasiliano ndani yake; Kusanifisha lugha ya Kiswahili kwa kutumia kwa ufasaha majina ya ngeli ya LI-YA.

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema | Yaliyomo | Mbinu za kufundishia na kujifunza |
|---|---|---|---|---|
| – Kufafanua dhima ya fasihi ya Kiswahili.<br><br>– Kuelezea maana ya kila tanzu ya fasihi ya Kiswahili.<br><br>– Kuonyesha mchango wa kila tanzu katika maendeleo ya kiutamaduni na kiuchumi ndani ya nchi.<br><br>– Kukumbuka matumizi sahihi ya Kiswahili kwa kuzingatia vipengele vya kisarufi kama vile matumizi ya majina ya ngeli ya LI-YA. | – Kujadili kimazungumzo na kimaandishi umuhimu wa fasihi katika jamii.<br><br>– Kuhusianisha fasihi na sanaa.<br><br>– Kutofautisha tanzu za fasihi simulizi na fasihi andishi.<br><br>– Kutunga na kujaza sentensi tofauti kwa kuzingatia matumizi ya majina ya ngeli ya LI-YA.<br>– Kusahihisha tungo tofauti zinazopatikana na makosa ya kisarufi kuhusu majina ya ngeli | – Kuipenda na kuikuza lugha ya Kiswahili.<br><br>– Kuimarisha fasihi kama kazi ya sanaa inayorahisisha mawasiliano katika jamii.<br><br>– Kutoa mchango wake binafsi katika maendeleo ya utamaduni na uchumi wa raia kwa kutumia tanzu tofauti za fasihi.<br><br>– Kuitumia fasihi kwa malengo chanya na kuepuka matumizi mabaya ya fasihi. | – Maana ya sanaa.<br><br>– Maana ya fasihi.<br><br>– Fasihi katika jamii, yaani umuhimu wa fasihi au nafasi ya fasihi katika jamii. Utangulizi wa nadharia ya fasihi ya Kiswahili, yaani fasihi simulizi na fasihi andishi kwa kuweka mkazo kwenye mifano ya tanzu za | -Wanafunzi watatoa maoni tofauti kuhusu:<br>– Mchango wa fasihi (nyimbo, hadithi, mashairi) katika maendeleo ya nchi ya Rwanda wakizingatia masuala kama amani, maridhiano, uzalendo, usawa wa kijinsia n.k.<br><br>– Sababu kuu za kutokuwa na tabia ya kupenda kusoma na kuandika nchini Rwanda.<br><br>– Kutafuta methali za kutosha katika Kinyarwanda ambazo zinabeba mada ya malezi bora katika ujenzi wa jamii ya Wanyarwanda na |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ya LI-YA. | | fasihi simulizi: hadithi, methali na nahau.<br>Sarufi: Matumizi ya ngeli za majina ya LI-YA pamoja na vivumishi vyake katika umoja na wingi.<br>Mfano:<br>- Jino langu linaniuma.<br>- Meno yangu yananiuma. | kuzilinganisha na za Kiswahili zinazohusiana.<br><br>– Majadiliano ya wanafunzi juu ya madhara ya fasihi inapotumiwa vibaya. Watumie mifano kutoka katika fasihi ya Kinyarwanda (nyimbo, methali, nahau) katika kipindi cha kabla ya mauaji ya kimbari yaliyotokea nchini Rwanda mnamo mwaka wa 1994.<br><br>– Wanafunzi watapewa majina kumi ya ngeli ya LI-YA na kuwaomba kuyatumia katika kifungu cha habari kifupi. |
| *Uhusiano wake na masomo mengine: Masomo yanayohusiana na utafiti wa kielimu, kihistoria, uandishi wa shahada kwa wanafunzi wanaojitahidi kumaliza masomo yao katika vyuo vikuu.* | | | | |
| *Vigezo vya tathmini au upimaji: Uwezo wa : kutaja tanzu za fasihi ya Kiswahili na mifano yake, kueleza dhima na kutetea umuhimu wa fasihi kwa jumla na ile ya Kiswahili katika kuiendeleza jamii, Kutumia ngeli ya LI- YA kwa usahihi.* | | | | |
| *Zana au vifaa: Vitabu, mtandao wa intaneti, runinga, majalida, taarifa zilizorikodiwa, vinasasauti, simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati, n.k.* | | | | |

| MADA KUU | MADA NDOGO | |
|---|---|---|
| **iii.UHAKIKI WA HADITHI ZA MASIMULIZI KATIKA KISWAHILI** | **MUHTASARI, FANI NA MAUDHUI** | **Idadi ya vipindi: 50** |

**Ujuzi upatikanao katika mada:** Kuelewa na kufuata mtindo wa kuandika muhtasari wa hadithi aliyoisikiliza au kuisoma; kuchambua hadithi za Kiswahili kwa kuzingatia fani na maudhui yanayojitokeza katika hadithi; kusimulia hadithi rahisi za masimulizi; kujua mabadiliko ya kisarufi katika matumizi ya majina ya ngeli ya PA-M-KU-.

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema | Yaliyomo | Mbinu za kufundishia na kujifunzia |
|---|---|---|---|---|
| – Kukumbuka mwongozo wa kufuata katika utoaji wa muhtasari wa hadithi.<br><br>– Kuorodhesha mambo muhimu yanayozingatiwa katika fani na maudhui wakati wa uchambuzi wa hadithi.<br><br>– Kutambua mabadiliko ya majina ya ngeli ya PA-M-KU toka umoja kwenda wingi kulingana na vivumishi tofauti vya majina haya. | – Kuchambua hadithi mbalimbali za Kiswahili kutokana na ujuzi wa uchambuzi aliopata.<br><br>– Kutoa tathimini ya hadithi aliyochambua kulingana na mtindo maalum wa uhakiki aliofuata.<br><br>– Kusimulia tena hadithi aliyowahi kusimuliwa au kuisoma.<br>– Kuandika muhtasari wa hadithi | – Kuonesha umoja na ushirikiano katika maisha<br>– Kufurahia utanzu wa hadithi na kujisikia hamu ya kuiga mazuri katika kazi za sanaa au fasihi.<br><br>– Kuendeleza akili yake katika mambo ya kujadili, kutoa tafakuri tunduizi, kutathimini,...<br><br>– Kujenga uwajibikaji katika maisha ya kila siku.<br><br>– Tabia ya kuzingatia | – Sifa za muhtasari wa habari.<br><br>– Mwongozo wa kutoa muhtasari mzuri, yaani taratibu zinazofuatiwa wakati wa kutoa muhtasari wa hadithi.<br><br>– Mambo muhimu ya kuzingatiwa wakati wa kufafanua fani na maudhui.<br><br>– Mfano wa uhakiki wa hadithi simulizi zenye msingi katika uzalendo, ushirikiano, maridhiano, mapenzi, uwajibikaji, n.k. | – Wanafunzi watunge hadithi kutokana na jina la hadithi linalotokana na methali waliyojichagulia wenyewe.<br>– Kila mwanafunzi afanye zoezi la kusimulia mbele ya darasa hadithi aliyoitunga<br>– Wanafunzi katika vikundi waandike muhtasari wa hadithi waliyoisikiliza au kuisoma.<br>– Wanafunzi watachambua hadithi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | aliyoisoma au kuisikiliza.<br>– Kutunga na kusahihisha sentensi sahihi kwa kuzingatia matumizi ya majina ya ngeli ya PA-M-KU-. | maelekezo na maagizo yatolewayo na wakubwa. | – Mfano wa uchambuzi wa hadithi kwa kutoa muhtasari, kuonyesha fani na maudhui.<br><br>– Sarufi: Matumizi ya majina ya ngeli ya PA-M-KU pamoja na vivumishi ambatana. | tofauti za Kiswahili na Kinyarwanda ambazo ndani yake hubeba mada ya kutoa maadili mema na kupigana dhidi ya ukatili katika jamii.<br><br>– Wanafunzi watapewa majina ya ngeli ya PA-M-KU na kuombwa kuyatumia katika vifungu vya habari vifupi. |
| *Uhusiano wake na masomo mengine: Masomo yanayohusiana na utafiti wa kielimu, kihistoria, uandishi wa shahada kwa wanafunzi wanaojitahidi kumaliza masomo yao katika vyuo vikuu.* | | | | |
| *Vigezo vya Tathmini au Upimaji: Uwezo wa: kuandika muhtasari wa hadithi, kutunga na kuchambua hadithi kwa kuzingatia fani na maudhui, kusimulia hadithi, kutumia kwa usahihi ngeli ya PA-M-KU- katika mawasilino.* | | | | |
| *Zana au vifaa: Vitabu, mitandao ya intaneti, majalida, rikoda, vinasa sauti, simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati.* | | | | |

| MADA KUU | MADA NDOGO | |
|---|---|---|
| **iv.UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO** | **MIDAHALO NA MIJADALA** | **Idadi ya vipindi: 49** |

**Ujuzi upatikanao katika mada:** Kuweza kuelewa mwongozo wa midahalo na mijadalo na kushiriki katika kazi za majadiliano kwa kuzingatia mada zilizotolewa kujadiliwa; kujiandaa na mdahalo kwa kutafiti na kuandika hoja atakazotumia, kujua jinsi ya kutoa amri kwa vitenzi.

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema | Yaliyomo | Mbinu za kufundishia na kujifunza |
|---|---|---|---|---|
| – Kuonesha uwezo wa kufanya mjadala kutokana na maandalizi ya awali yaliyoegemea katika utafiti.<br>– Kukumbuka taratibu za kufuata wakati wa kutoa hoja katika makundi.<br>– Kutafsiri mazingira ya mada na kuijadilia bila upotovu wowote.<br>– Kutambua lugha inayofaa katika majadiliano.<br>– Kuelezea mtiririko | – Kujiandaa awali kabla ya mdahalo kwa utafiti na kupangilia hoja za mdahalo.<br>– Kuonyesha upande wa kuegamia katika kutoa hoja zake (mtetetezi au mpinzani).<br>– Kutoa suluhisho katika majadiliano kwa kutetea hoja zinazomkera.<br>– Kutumia lugha sahihi na yenye kuvutia na kuridhisha.<br>– Kutumia ishara za mwili kulingana na | – Kuonesha moyo wa heshima wakati wa majadiliano.<br>– Kutokata tamaa na kutokasirika ovyo.<br>– Ushirikiano.<br>– Urafiki.<br>– Kujiamini.<br>– Kushindana kwa hoja bila kupigana au kugombana.<br>– Kukubali kutokubalina na kuheshimu mawazo ya watu wengine’ | – Maana ya mjadala na mdahalo.<br>Mambo ya kuzingatiwa katika maandalizi ya awali ya kufanikisha ushiriki wa mdahalo kwa ufanisi.<br>– Mwongozo wa mdahalo/mjadala, yaani taratibu za kufuata wakati wa kushiriki kwenye mdahalo na mjadala.<br>– Mfano wa mdahalo na mjadala kuhusu mada izungumziayo kazi | – Wanafunzi watumie kamusi sanifu ya Kiswahili au mtandao wa intaneti kwa kuchunguza maana ya mdahalo na mjadala.<br>Wanafunzi wapewe nafasi ya kwenda kufanya utafiti na maandalizi juu ya mada watakazofanyia mdahalo<br>– Wanafunzi katika vikundi wapewe mada moja lakini kila kundi lielekezwe kuwa na mtazamo tofauti na kundi jingine kisha wajiandae kwa ajili ya kushiriki mdahalo na majadiliano. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| wa hoja au majadiliano ili kujiepusha na marudio ya wazo au fikra.<br><br>– Kuelezea jinsi ya kutoa amri kwa kutumia hali ya kushurutisha kwa vitenzi. | hoja inayohusika. | – Kusikiliza mawazo ya watu wengine hata kama hawakubaliani nayo. | maalum zinazotakiwa kufanywa na watu wa kiume na nyingine kufanywa na watu wa kike.<br><br>– Sarufi: Hali ya kushurutisha kwa vitenzi umoja na wingi.<br>Mfano: Njoo na njooni Kimbia na kimbieni, n.k. | – Kwa njia ya mijadala, wanafunzi watazungumzia mada zihusuzo:<br>a) mchango wa wazazi katika malezi ya watoto wao.<br><br>b) mtindo wa kisiasa wa " maelezi kwa wote" ambao unamwamrisha kila mtoto kuingia shuleni.<br><br>c) Masuala yanayoiangamiza jamii kama vile madawa ya kulevya, ugonjwa wa malaria, ukimwi, n.k.<br><br>– Kupatiwa vitenzi tofauti na kuombwa kutunga sentensi kwa kutumia hali ya kushurutisha. |
| *Uhusiano wake na masomo mengine: Masomo yanayohusiana na michezo, masomo ya kujenga ushirikiano, umoja, adabu, n.k.* | | | | |
| *Vigezo vya tathmini au upimaji: Uwezo wa: kufanya maandalizi ya awali kwa ajili ya midahalo na majadiliano, kushiriki katika utetezi wa ukweli au jambo fulani katika kundi la watu kwa njia ya majadiliano, kuandika hoja za pande zote zilizojitokeza katika majadiliano, kuandika hitimisho la jumla kuhusiana na majadiliano au mdahalo.* | | | | |
| *Zana au vifaa: Meza duala, redio, runinga, taarifa zilizorikodiwa, vifaa vya kunasia sauti, simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati.* | | | | |

| MADA KUU | MADA NDOGO | |
|---|---|---|
| v. UTUNGAJI | INSHA ZA MASIMULIZI AU KUBUNI NA UANDISHI WA RIPOTI | Idadi ya vipindi: 51 |

**Ujuzi upatikanao katika mada:** Kumwezesha mwanafunzi kuzingatia mwongozo wa kutunga insha za masimulizi kulingana na mada iliyotolewa na kuzitolea muhtasari darasani kwa njia ya mazungumzo; Kuandika ripoti rahisi; kuelewa jinsi ya kumnukuu mtu mwingine.

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema | Yaliyomo | Mbinu za kufundishia na kujifunza |
|---|---|---|---|---|
| – Kuelezea tofauti iliyopo kati ya insha ya kubuni na hadithi ya masimulizi.<br><br>Kueleza mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa ripoti.<br><br>– Kukumbuka sehemu kuu za kuzingatia katika utungaji wa insha za masimulizi.<br><br>– Kutambua taratibu za kutoa ripoti ya taarifa kwa kuzingatia usemi asili na usemi wa | – Kutunga insha ya masimulizi kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa.<br><br>– Kutayarisha na kutoa muhtasari wa insha bila kupotosha ukweli wa mwandishi.<br><br>– Kuandika ripoti kuhusu ziara waliyoifanya au ripoti kuhusu kongamano la lugha ya Kiswahili waliloshiriki | Kutokana na mada ya insha, mwanafunzi ataathiriwa katika nyanja tofauti:<br>- Atafuata maadili mema ya kuwa na adabu, usafi, kupigana na wivu, uvivu, ukatili, uzinifu, ulevi, ujinga, umasikini, n.k.<br>- Ataridhika na kazi ya ubunaji katika maisha yake.<br>-Kuonyesha ubunifu wa hali ya juu katika kujadili mambo mbalimbali na kutatua matatizo. | – Maana ya insha kwa ujumla.<br><br>– Aina za insha.<br><br>– Maana ya insha za masimulizi.<br><br>– Mwongozo wa insha za masimulizi, yaani taratibu za kuzingatia katika utungaji wa insha: utangulizi, kiini cha insha pamoja mwisho.<br><br>– Mfano wa insha za masimulizi kuhusu mada ifuatayo: | – Wanafunzi watasoma insha mbalimbali za masimulizi kutoka vitabu tofauti na kuzifanyia mhadhara darasani.<br><br>– Watatunga insha za masimulizi kuhusu mada mbalimbali. Mfano: safari, ugonjwa wa ukimwi, kazi za umuganda, usafi, madawa ya kulevya, uvivu, utawala bora, umoja wa jamii, afya, n.k.<br><br>– Wanafunzi katika vikundi vyao watashiriki katika kuandika ripoti juu ya jambo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| taarifa.<br><br>– Kubainisha mabadiliko yaliyopo toka usemi asili kwenda usemi wa taarifa. | – Kutoa ripoti ya taarifa ya habari aliyosikiliza au aliyoisoma mahali fulani kwa kutumia usemi wa taarifa. | | Matarajio yangu baada ya kumaliza masomo yangu ya shule za sekondari.<br><br>Maana ya ripoti.<br><br>Aina za ripoti.<br><br>Mwongozo wa namna ya kuandika ripoti juu ya masuala rahisi na yanayoendana na maisha ya wanafunzi<br><br>– Sarufi: Usemi asili na usemi wa taarifa. | litakalopendekezwa kwa pamoja na mwalimu pamoja na wanafunzi<br><br>– Kusikiliza redio au runinga na kutoa ripoti ya habari waliyofuata kwa kuzingatia usemi wa taarifa.<br><br>– Kupewa tungo katika usemi asili na kuzibadilisha katika usemi wa taarifa. |
| – *Uhusiano wake na masomo mengine: Masomo yanayohusiana na ubunaji, kujenga mahusiano mema, kujenga tabia njema, umoja na ushirikiano, umoja na maridhiano, mapendo, adabu, siasa, dini, afya, n.k.* | | | | |
| – *Vigezo vya tathmini au upimaji: Uwezo wa kuandika ripoti, kutunga insha za kutosha juu ya mada mbalimbali kuhusu masuala ya kiulimwengu; kuripoti taarifa mbalimbali kama ilivyosemwa na msemaji.* | | | | |
| – *Zana au vifaa: Vitabu, mitandao ya intaneti, majalida, taarifa zilizorikodiwa, redio, runinga, simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati.* | | | | |

### 5.3. Kidato cha tano

#### 5.3.1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha tano

Inatazamiwa kwamba mwanafunzi amalizapo kidato cha nne ataweza:

- Kuwasiliana kwa mazungumzo na maandishi na watu au jamii katika miktadha mbalimbali.
- Kufanya utungaji na ubunaji wa kazi za fasihi na zisizo za kifasihi kwa ufasaha.
- Kufanya ufafanuzi wa kina wa kila utanzu uliopo katika fasihi ya Kiswahili.
- Kusoma na kuhakiki kazi za fasihi simulizi na fasihi andishi.
- Kuainisha na kubainisha tanzu za fasihi ya Kiswahili na kueleza dhima ya fasihi katika jamii.
- Kufanya mawasiliano rasmi kwa ufasaha akizingatia malengo na nyenzo ya mawasiliano inayotumika.
- Kusikiliza, kusoma na kuelewa kwa kina taarifa au habari mbalimbali kutokana na vyanzo vya habari zinazohusu masuala ya jamii za kimasimulizi na kimaandishi.

### 5.3.2. Muhtasari wa kidato cha tano

| MADA KUU | MADA NDOGO | | | |
|---|---|---|---|---|
| **i.UWANJA WA FASIHI KAMA SANAA** | **Nadharia ya Fasihi Simulizi katika Kiswahili na Tanzu zake** | | **Idadi ya vipindi:65** | |
| **Ujuzi upatikanao katika mada**: Mwanafunzi aweze kufafanua tanzu za Fasihi katika Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuindeleza jamii au nchi yake. | | | | |
| **Malengo ya kujifunza** | | | | |
| **Maarifa na ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | **Yaliyomo** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia.** |
| – Kuelezea fasihi ya Kiswahili na udhamini wa kazi za kifasihi.<br><br>– Kutambua na kuzielezea tanzu mbalimbali za fasihi simulizi (semi, masimulizi, ushairi, mazungumzo).<br><br>– Kujadili | – Kufafanua kwa kina tanzu na vipera vya fasihi simulizi.<br><br>– Kuzipangilia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi katika Kiswahili katika makundi yake muhimu.<br><br>– Kutumia methali na nahau za Kiswahili akizihusisha na maisha ya kila siku. | – Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br><br>– Kuithamini fasihi na kuonesha hamu kuwa msanii. | – Maana ya fasihi katika Kiswahili.<br><br>– Udhamini katika fasihi katika Kiswahili.<br><br>– Ufafanuzi wa kina wa tanzu za fasihi simulizi katika Kiswahili na vipera vyake kama vile semi, mazungumzo | – Wanafunzi wabainishe katika vikundi juu ya matini ambazo ni za kifasihi na zisizo.<br><br>– Wanafunzi katika vikundi wajadiliane au kubainisha juu ya faida na athari ya udhamini katika kazi za fasihi.<br><br>– Wanafunzi waainishe matini waliyopewa kwa kuzingatia jina sahihi la tanzu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mchango wa fasihi katika Kiswahili na jamii.<br><br>– Kubainisha aina za sentensi za Kiswahili. | – Kusimulia hadithi au shairi darasani.<br><br>– Kuchambua sentensi za Kiswahili kwa kuonesha kutokana na aina zake. | | na masimulizi zilivyozingatiwa.<br><br>– Mifano ya kutosha ya nyimbo, methali, nahau na vitendawili pamoja na maana au majibu yake.<br><br>– Ushairi simulizi wa Kiswahili.<br>- Maana ya yake<br>- Aina zake<br>- Mifano yake<br>- Dhima yake katika jamii<br><br>- Sarufi: Aina za sentensi za Kiswahili : Sentensi sahili, sentensi ambatano, sentensi changamano... | au kipera.<br><br>– Wanafunzi katika makundi wapange vipera vya tanzu mbalimbali za fasihi simulizi katika tanzu zake.<br><br>– Kusoma na kuandika maelezo mafupi kuhusu ufafanuzi wa tanzu na vipera mbalimbali kwa kutumia marejeleo waliyoelekezwa na mwalimu.<br><br>– Wanafunzi wafanye kazi ya kukusanya tanzu na vipera mbalimbal vya fasihi simulizi na kuwasilisha darasani.<br><br>– Kusimulia darasani hadithi waliyoisikia nyumbani au mahali pengine. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | – Kuhusisha methali za Kiswahili na za Kinyarwanda na kuelezea mazingira yake (jinsi zinavyotumiwa).<br><br>– Kutunga shairi kuhusu mada mbalimbali, kulikariri na kulisimulia darasani.<br><br>– Kujadili kwa njia ya mdahalo athari za ushairi simulizi wa Kinyarwanda katika maendeleo ya jamii ya Wanyarwanda. |

| |
|---|
| *Uhusiano wake na masomo mengine: Mbali na lugha nyingine, somo hili linahusiana na masomo ya utamaduni, malezi bora, ufundi na ubunaji.* |
| *Vigezo vya tathmini au upimaji: Uwezo wa: Kutaja bila kusita tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiswahili pamoja na mchango wake katika jamii; kufafanua tanzu za fasihi simulizi; kutumia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi katika maisha ya kila siku; Kutumia aina mbalimbali za sentensi za Kiswahili kwa usahihi afanyapo mawasiliano.* |
| *Zana/vifaa: Vitabu vya fasihi, tanzu za fasihi zilizorikodiwa, mchoro wa sanaa na matawi yake, matini na majarida yanayoelezea mwanzo na maendeleo ya fasihi, mtandao wa intaneti.* |

| MADA KUU | MADA NDOGO | |
|---|---|---|
| **ii.UHAKIKI NA UWASILISHAJI KATIKA FASIHI SIMULIZI** | **FANI NA MAUDHUI KATIKA FASIHI SIMULIZI** | **Idadi ya vipindi: 65** |

**Ujuzi upatikanao katika mada**: Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili.

| **Malengo ya kujifunza** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Maarifa na Ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | **Yaliyomo** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia** |
| – Kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa tanzu za fasihi simulizi.<br><br>– Kuonesha uwezo wa kuwasilisha mada inayohusiana na uhakiki wa tanzu za fasihi simulizi.<br><br>– Kuelezea hadharani | – Kutumia vipengele vya fani na maudhui katika kuhakiki tanzu mbalimbali za fasihi simulizi.<br><br>– Kutathmini ubora wa utanzu wa fasihi simulizi kwa kuzingatia fani na<br><br>–<br><br>– maudhui.<br><br>– Kuwasilisha mbele ya darasa uchambuzi wa utanzu wowote wa fasihi simulizi. | – Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tanduizi.<br><br>– Uhuru wa kutoa hoja au maoni tofauti na ya mwingine bila ugomvi wowote.<br><br>– Mabadiliko au athari chanya za kiakili na kitabia<br>– kutokana na ujumbe unaozingatiwa katika tanzu iliyoshughulikiwa. | – Maana ya uhakiki na vipengele vya uhakiki katika utanzu wa fasihi simulizi.<br><br>– Mwongozo wa uhakiki wa tanzu za fasihi simulizi kwa kuzingatia fani na maudhui. Tanzu za kuzingatiwa ni: (hadithi, methali, vitendawili, nahau n.k.)<br><br>– Mwongozo wa kutoa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi iliyosomwa au kusikilizwa na mwanafunzi. Kwa | – Katika makundi madogo madogo, wanafunzi watachagua tanzu tofauti za fasihi simulizi, baada ya kusoma na kuelewa watazitolea uhakiki kwa kuzingatia mwongozo wa uchambuzi uliotolewa.<br><br>– Wanafunzi katika vikundi watawasilisha uhakiki walioufanya juu ya utanzu wa fasihi simulizi.<br><br>– Wanafunzi katika makundi watasikiliza |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| maoni yake kuhusu utanzu wa fasihi simulizi aliousoma au kuusikiliza darasani kwa kueleza alichofurahia, chukia, jifunza n.k).<br><br>– Kukumbuka mambo muhimu ya muundo wa sentensi ya Kiswahili. | – Kulinganisha tanzu moja na nyingine kwa kueleza kufanana na kutofautiana katika vipengele vya fani na maudhui.<br><br>– Kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi zinavyojitokeza katika tanzu za fasihi simulizi kama vile masimulizi na mazungumzo.<br><br>– Kuchambua sentensi za Kiswahili kwa kuonyesha muundo wake. | – Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | mfano nini kimemfurahisha au kumchukiza.<br><br>– Mwongozo wa kutoa uwasilishaji (mhadhara) kuhusu kazi ya fasihi iliyoshughulikiwa, yaani taratibu za kufuata wakati wa kutoa uwasilishaji.<br><br>– Sarufi: Muundo wa sentensi za Kiswahili : Kiima, kiarifa, shamirisho na chagizo… | au kusoma utanzu wowote wa fasihi simulizi kisha wajibu maswali kuhusu maoni yao binafsi juu ya utanzu husika.<br><br>– Katika makundi, wanafunzi watashughulikia ubunaji wa mojawapo ya tanzu za fasihi zilizotajwa hapo juu, baadaye kila kundi litabadilishana na kundi jingine kwa ajili ya kuhakiki kazi hizo zilizofanywa na kuzitolea tathimini darasani. |
| *Uhusiano wake na masomo mengine: Somo hili linahusiana na masomo mengine yanayoshughulikia mila na utamaduni wa jamii, mambo ya sanaa, michezo, utafiti, historia, n.k.* | | | | |
| *Vigezo vya tathmini au upimaji: Uwezo wa: Kuchambua au kuhakiki tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiswahili akizingatia mbinu za uhakiki alizojifunza; kuwasilisha mbele ya darasa uhakiki alioufanya; Kuzingatia miundo sahihi ya sentensi za Kiswahili katika mawasiliano; kubuni walau kazi ya fasihi yenye muundo rahisi na fupi.* | | | | |
| *Zana/vifaa: Vitabu vya fasihi, magazeti, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti.* | | | | |

| MADA KUU | MADA NDOGO | | | |
|---|---|---|---|---|
| **III.MAWASILIANO RASMI** | **Utungaji wa barua rasmi, simu na matangazo** | | **Idadi ya vipindi: 72** | |
| **Ujuzi upatikanao katika mada:** Kumwezesha mwanafunzi kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandiko rasmi akitumia Kiswahili sanifu. | | | | |
| **Malengo ya kujifunza** | | | | |
| **Maarifa na Ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | **Yaliyomo** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia** |
| -Kueleza tofauti iliyopo baina ya barua ya kirafiki na barua rasmi.<br><br>-Kukumbuka sehemu muhimu za barua rasmi.<br><br>-Kutoa mfano wa mazingira barua za kikazi, simu pamoja na | -Kutunga barua ya kikazi kutokana na kisa kinachojitokeza.<br><br>-Kuonyesha kwa mchoro sehemu kuu za barua rasmi.<br><br>-Kuandika simu kwa kuzingatia taratibu au mtindo unaojidhihilisha. | -Adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaoawasiliana nao.<br><br>-Ari ya kupenda kuwasiliana na watu kwa kutumia njia tofauti za mawasiliano.<br><br>-Moyo wa kujenga urafiki na ushirikiano na watu mbalimbali | -Barua rasmi:<br><br>-Mazingira ya barua rasmi, yaani mahali zinapotumiwa.<br><br>-Mwongozo wa kutunga barua za kikazi (sehemu kuu za barua ya kikazi pamoja na taratibu za kufuata).<br><br>-Mfano wa barua ya kikazi kuhusu ombi la kazi ya ualimu.<br><br>-Simu:<br><br>-Aina za simu | Katika kundi la wanafunzi wawili mawili, mwanafunzi mmoja (kama mwandishi) atatunga barua rasmi kuhusu kisa fulani na wa pili (mwandikiwa) atamjibu kulingana na ombi linalohusika<br><br>Katika kundi la wanafunzi wawili mawili, mwanafunzi mmoja atampelekea mwenzie ujumbe wa simu kwa niaba ya kiongozi wake na mwingine atatoa jibu<br><br>Katika makundi makundi, wanafunzi watatayarisha |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| tangazo lilotumiwa.<br><br>-Kutambua mtindo wa simu na wa tangazo<br><br>-Kuonyesha njia tofauti za uchanganuzi wa sentensi ya Kiswahili. | -Kutayarisha tangazo maalumu kulingana na mazingira yanayotolewa. | kwa njia ya mawasiliano. | -Mwongozo wa kutunga simu(sehemu kuu za simu pamoja na taratibu za kufuata).<br><br>-Mfano wa simu za maneno (telegramu) mtu fulani akimwomba mwenzake ampelekee pesa kwa njia ya fedha mkono (Mobile money).<br><br>-Matangazo:<br><br>-Aina za matangazo<br><br>-Mwongozo wa utungaji wa matangazo (sehemu kuu za tangazo pamoja na taratibu za kufuata)<br><br>-Mfano wa tangazo kuhusu madawa ya kulevya.<br><br>-Sarufi:<br><br>Uchanganuzi wa sentensi ya Kiswahili: | matangazo mbalimbali kutokana na visa tofauti vitakavyotolewa.<br><br>Wanafunzi watachanganua tungo mbalimbali kwa kuonyesha njia ya upambanuzi iliyofuatiliwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | -Njia ya matawi<br><br>-Njia ya mishale<br><br>-Njia ya jedwali. | |
| | -Kuchanganua sentensi mbalimbali za Kiswahili kwa njia tofauti. | | | |

***Uhusiano wake na Masomo Mengine**: Somo hili linahusiana na somo la Mawasiliano katika nyanja mbalimbali (ofisini, biashara, siasa, n.k.)*

***Vigezo vya Tathmini au Upimaji**: Uwezo wa kutunga barua, simu na matangazo kulingana na mazingira husika*

***Zana/vifaa**: Matini zenye mitindo mbalimbali ya uandishi wa barua, magazeti, mtandao wa internet, vitabu, simu ya mkononi.*

<table>
<tr><td colspan="2">MADA KUU</td><td colspan="3">MADA NDOGO</td></tr>
<tr><td colspan="2">iv.KUSOMA NA KUTAFSIRI</td><td colspan="2">UFAHAMU NA UFUPISHO</td><td>Idadi ya vipindi: 72</td></tr>
<tr><td colspan="5">Ujuzi upatikanao katika mada: Kuwezesha mwanafunzi kusoma vifungu vya habari, kuvitafsiri na kuvitolea ufupisho.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Malengo ya kujifunza</td><td colspan="2"></td></tr>
<tr><td>Maarifa na Ufahamu</td><td>Stadi</td><td>Maadili na mwenendo mwema</td><td>Yaliyomo</td><td>Mbinu za kufundishia na kujifunzia</td></tr>
<tr><td>-Kuelezea mbinu za kufahamu kifungu cha habari fulani.<br>-Kutaja sifa za ufupisho mzuri.<br>-Kujadili kanuni za ufupisho wa habari fulani.<br>-Kutoa maana inayopatikana katika aya za kifungu cha habari bila kuyapotosha.</td><td>-Kujibu maswali kwa ufasaha yanayojitokeza katika kifungu cha habari kinachohusika.<br>-Kuonyesha dhamira kuu au kiini cha habari kinachozungumziwa.<br>-Kuonyesha sehemu kuu za kifungu cha habari na dhamira zake.<br>-Kufupisha vifungu vya habari kwa kufuata</td><td>-Ukuzaji wa tafakuri tunduizi<br>-Ukomavu wa akili kwa kuyatafsiri maoni ya wengine.<br>-Utimizaji wa wajibu katika mbinu za kulitatua tatizo fulani.</td><td>-Taratibu au mbinu za kufahamu kifungu cha habari.<br>-Mfano wa kifungu cha habari kuhusu usafi wa mwili pamoja na maswali ya ufahamu.<br>-Mbinu za kufupisha kifungu cha habari.<br>Ufupisho wa kifungu cha habari husika hapo juu<br>-Sarufi: Muhtasari (kwa njia ya jedwali) wa matumizi ya</td><td>-Katika makundi, wanafunzi watapewa vifungu tofauti vya ufahamu na kuombwa kujibu maswali ya ufahamu yatakayojitokeza.<br>-Katika makundi, wanafunzi watajishughulisha na ufupisho wa vifungu vya habari walivyosoma na kufahamu, kisha</td></tr>
</table>

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| -Kukumbuka na kuzingatia mabadiliko yanayojitokeza katika matumizi nyakati za kiswahili katika hali yakinishi na hali kanushi. | mwongozo wa ufupisho. | | nyakati zilizoshughulikiwa (wakati uliopo, uliopita, ujao, mtimilifu, wa mazoea na wa masharti) katika hali yakinishi na hali kanushi. | wasimulie darasani kazi waliyofanya.<br><br>Wanafunzi watasikiliza (nyumbani au mahali pengine) habari kwenye redio au televisheni na kuzitolea ufupisho au muhtasari kwa njia ya maandishi na mazungumzo. |
| ***Uhusiano wake na Masomo mengine***:*Somo hili linahusiana na somo lolote linaloshughulikia maswala ya jamii na ulimwengu kwa ujumla.* | | | | |
| ***Vigezo vya Tathmini au Upimaji***: *Kazi na mazoezi ya kutosha yahusuyo ufahamu na ufupisho kwa ajili ya kumwezesha mwanafunzi kuwa na uelewevu kamili wa kufahamu na kufupisha habari mbalimbali.* | | | | |
| ***Zana/vifaa***: *Matini zenye habari mbalimbali, taarifa, kanda na vinasa sauti.* | | | | |

### 5.4. Kidato cha sita

#### 5.4. 1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha sita

Inatazamiwa kwamba mwanafunzi amalizapo kidato cha sita ataweza:

- Kuwasiliana Kwa mazungumzo na maandishi na watu au jamii katika miktadha mbalimbali.
- Kufanya utungaji na ubunaji wa kazi za fasihi na zisizo za kifasihi kama vile hotuba.
- Kufanya ufafanuzi wa kina wa vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa fasihi.
- Kusoma na kuhakiki kazi za fasihi andishi.
- Kushiriki katika midahalo kuhusu mada mbalimbali kwa ufasaha akitumia Kiswahili sanifu.
- Kufanya ufupisho wa matini za kifasihi na zisizo za kifasihi.
- Kusikiliza, kusoma na kuelewa kwa kina taarifa au habari mbalimbali kutokana na vyanzo vya habari zinazohusu masuala ya jamii za kimasimulizi na kimaandishi.

### 5.4.2. Muhtasari wa kidato cha sita

| MADA KUU | MADA NDOGO | |
|---|---|---|
| **i.FASIHI KATIKA KISWAHILI** | **UFAFANUZI WA TANZU ZA FASIHI ANDISHI KATIKA KISWAHILI** | **Idadi ya vipindi: 65** |

**Ujuzi upatikanao katika mada:** Kuelewa tanzu tofauti za fasihi andishi katika Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa na kuitumia kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani.

| Malengo ya kujifunza | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Maarifa na ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | **Yaliyomo** | **Mbinu za kufundishia na kujifunza** |
| – Kutaja tanzu za fasihi andishi ya Kiswahili.<br>– Kufafanua maana ya kila tanzu ya fasihi andishi.<br>– Kueleza mchango wa kila tanzu katika maendeleo ya kiutamaduni na kiuchumi ndani ya nchi.<br>– Kubainisha mtindo wa tanzu za fasihi andishi kwa kuzingatia fani yake.<br>– Kuelezea vifungu vya sentensi. | – Kuigiza tanzu za fasihi andishi zinazohusika.<br>– Kulinganisha tanzu mbalimbali za fasihi andishi kutokana na muundo wa kila tanzu.<br>– Kujadili mchango wa fasihi andishi katika maendeleo ya kiutamaduni, kijamii na kiuchumi katika nchi.<br>– Kusoma au kusikiliza kazi za fasihi kutoka | Mwanafunzi atapata mabadiliko ya:<br>– Kuuhifadhi utamaduni wa nchi na kuukuza zaidi kutokana na tabia za wahusika zilizojitokeza katika tanzu husika.<br>– Kuimarisha kazi za sanaa kama mojawapo ya | – Sifa za fasihi andishi na umuhimu wake.<br>– Ufafanuzi wa tanzu za fasihi andishi za Kiswahili :<br>- Hadithi fupi<br>- Riwaya<br>- Tamthilia<br>- Ushairi andishi.<br>– Mfano kwa kila tanzu husika.<br>– Sarufi: Vifungu vya sentensi: Mtindo wa | – Wanafunzi wapatiwe maandishi tofauti (vitabu, habari zilizorekodiwa, majarida, ...) yanayobeba ndani yake tanzu za fasihi andishi za Kiswahili na kuyaelezea.<br>– Kuigiza jukwani tamthilia itakayochaguliwa na mwalimu au wanafunzi wenyewe.<br>– Kulikariri shairi fulani na kulighani darasani.<br>– Wanafunzi wajadilie athari za tamthilia za Kinyarwanda |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | tanzu za fasihi andishi.<br><br>– Kutafsiri tabia za wahusika katika tanzu husika.<br><br>– Kuhalalisha uhusiano uliopo baina ya kichwa cha tanzu na yaliyomo.<br><br>Kuchambua sentensi za Kiswahili kwa kuonyesha vifungu vyake. | njia za kujitegemea maishani.<br><br>– Kutoa mchango wake binafsi katika mabadiliko ya maendeleo ya utamaduni na uchumi wa raia. | virai na vishazi. | (k.m. Urunana) katika kuimarisha hatua za kujikinga dhidi ya ugonjwa wa ukimwi (HIV/AIDS).<br><br>– Wapatiwe tungo mbalimbali za Kiswahili na kuwaomba kuzichambua kwa kuzitolea vifungu vyake. |
| *Uhusiano wake na masomo mengine: Masomo ya sanaa, kujenga uhusiano mwema, kujenga tabia njema, umoja na ushirikiano, umoja na maridhiano, mapendo, adabu, n.k.* | | | | |
| *Vigezo vya tathmini au upimaji: Uwezo wa kutofautisha aina mbalimbali za fasihi andishi kutokana na muundo wake.* | | | | |
| *Zana au vifaa: Vitabu, majalida, rikoda, vinasa sauti, simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati, mtandao wa intaneti.* | | | | |

| MADA KUU | MADA NDOGO | |
|---|---|---|
| **ii.FASIHI KATIKA KISWAHILI** | **UHAKIKI WA TANZU ZA FASIHI ANDISHI** | **Idadi ya vipindi: 65** |

**Ujuzi upatikanao katika mada:** Kuelewa na kufuata mtindo wa kuchambua hati za fasihi (vitabu, mashairi, nyimbo, ....) kwa minajili ya kukuza uelevu wa undani wa lugha na kutambua ujumbe unaojidhihirisha katika maendeleo ya fikra na utamaduni wa wananchi; kujua jinsi ya kunyumbua kitenzi cha Kiswahili.

| Malengo ya kujifunza | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Maarifa na ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | **Yaliyomo** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia** |
| – Kukumbuka utaratibu na hatua za kufuatwa wakati wa kuhakiki tanzu za fasihi andishi.<br><br>– Kuelezea athari za tanzu zilizoshughulikiwa kwa maisha ya jamii iliyolengwa.<br><br>– Kutambua tofauti iliyopo kati ya tanzu za fasihi simulizi na tanzu za fasihi andishi wakati wa kuhakiki.<br><br>– Kunukuu sehemu fulani fulani za kazi ya sanaa inayohusika kwa kukamilisha tathimini | – Kuchambua au kuhakiki tanzu mbalimbali za fasihi andishi ya Kiswahili kutokana na ujuzi wa kuchambua alioupata.<br><br>– Kutoa tathimini ya tanzu ya fasihi andishi fulani aliyochambua kulingana na vipengele vya fani na maudhui.<br><br>– Kutoa pendekezo kuhusu tabia za wahusika na athari zao katika ujenzi wa jamii.<br><br>– Kuhusianisha kichwa cha tanzu au jina la | – Mwanafunzi ataridhika na mtindo wa tanzu aliyochambua na kujisikia hamu ya kuiiga katika kazi za sanaa atakazoshughuliki a kama msanii.<br><br>– Mwanafunzi pia ataendeleza akili zake katika mambo ya kujadili, kutoa tafakuri tunduizi, kutathimini,...<br><br>– Kukuza na kuendeleza | – Mwongozo wa kuchambua tanzu za fasihi andishi (kulingana na aina yake):<br><br>1. Aina ya kazi andishi inayohusika<br>2. Wahusika<br>3. Maudhui na dhamira<br>4. Mandhari<br>5. Mbinu za lugha.<br><br>– Mfano wa uhakiki wa tamthilia, riwaya, hadithi fupi na mashairi ya moja wandishi mashuhuri | – Wanafunzi (katika makundi) watapatiwa maandishi tofauti (vitabu, habari zilizorikodiwa, majarida, ...) yanayobeba tanzu za fasihi andishi za Kiswahili na kutoa uchambuzi wake kwa kufuata mwongozo wa uchambuzi uliotolewa.<br><br>Watoe mhadhara wa kazi iliyofanywa na kuipatia hadhira fursa ya kutoa maswali au maoni yake.<br><br>– Watoe mapendekezo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| yake.<br><br>– Kutambua viambishi vya kitenzi kwa njia ya mnyambuliko. | kitabu alichosoma na yaliyomo na kisha kuhalalisha uteuzi wa jina hilo.<br><br>– Kutoa hitimisho kwa kulinganisha matukio yaliyojitokeza katika tanzu iliyoshughulikiwa na ukweli unaojidhihirisha leo. | utamaduni wa jamii za Kiafrika.<br><br>– Kujenga shauku na hatimaye kuingia katika dunia ya ubunaji wa fasihi andishi. | wa Kiswahili wanaojadili mambo yaendanayo na maisha na matarajio ya jamii ya Wanyarwanda.<br><br>– Sarufi: Mnyambuliko wa vitenzi | na hitimisho kuhusu kazi waliyoshughulikia.<br><br>– Wajadili tamthilia za Kinyarwanda (mfano wa Museke Weya) wakisisitizia juu ya wahusika na tabia zao katika harakati za kuboresha umoja na maridhiano wa Wanyarwanda.<br><br>– Kupatiwa kifungu cha habari kitakachobeba vitenzi tofauti na kuvitolea mnyumbuliko. |

| |
|---|
| *Uhusiano wake na masomo mengine: Masomo yanayohusiana na utafiti wa kielimu, kihistoria, uandishi wa shahada kwa wanafunzi wanaojitahidi kumaliza masomo yao katika vyuo vikuu.* |
| *Vigezo vya tathmini au upimaji: Uwezo wa kuchambua tanzu ya fasihi andishi kulingana na mwongozo wa uchambuzi aliojifunza.* |
| *Zana au vifaa: Vitabu, majarida, rikoda, vinasa sauti, simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati, mtandao wa intaneti.* |

| MADA KUU | | MADA NDOGO | | |
|---|---|---|---|---|
| iii.UBUNAJI | | iii..HOTUBA NA UFUPISHO | | Idadi ya vipindi: 62 |
| **Ujuzi upatikanao katika mada:** Mwanafunzi ataweza kuelewa mtindo wa hotoba na kuuzingatia katika mazoezi ya utungaji pamoja na ufupisho; kujua kuchambua kitenzi kwa njia ya uambishaji. | | | | |
| **Malengo ya kujifunza** | | | | |
| **Maarifa na ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | **Yaliyomo** | **Mbinu za kufundishia na kujifunza** |
| – Kuelezea tofauti iliyopo kati ya insha na hotuba.<br><br>– Kutaja sehemu kuu za hotuba.<br><br>– Kukumbuka mwongozo wa kutunga hotuba na ufupisho.<br><br>– Kutoa mfano wa sifa za hotuba na ufupisho.<br><br>– Kuonesha jinsi kitenzi kinavyoweza kuongezewa viambishi zaidi kwa njia ya uambishaji. | – Kutathimini hotuba kulingana na sifa zake.<br><br>– Kulinganisha hotuba na insha au hotuba fulani kwa hotuba nyingine.<br><br>– Kuendeleza hotuba kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa.<br><br>– Kufupisha hotuba inayohusika.<br><br>– Kulinganisha ufupisho uliotolewa kutoka makundi tofauti.<br><br>– Kuongezea mzizi wa | Kutokana na mada ya hotuba, mwanafunzi ataathiriwa katika nyanja tofauti. Kwa mfano: atafuata maadili mema ya kuwa na adabu, usafi, kupigana na wivu, uvivu, ukatili, uzinifu, ulevi, ujinga, umasikini, n.k. | – Sifa za hotuba.<br><br>– Mwongozo wa kutunga hotuba, yaani muundo wa hotuba kwa kuzingatia sehemu zake muhimu: anwani, utangulizi, mwili, tamati au mwisho...<br><br>– Mfano wa hotuba (kuhusu ushirikiano wa kijinsia) na uchambuzi wake kwa kuonyesha sehemu kuu pamoja na dhamira kuu za kila sehemu.<br><br>– Sifa za ufupisho na mbinu muhimu za kuzingatia katika ufupisho. | – Kutokana na mada tofauti (umoja wa Wanyarwanda, unyanyasaji wa kijinsia, kazi za umuganda, usafi wa mazingira, n.k.) wanafunzi watatunga hotuba na kuzisimulia hadharani.<br><br>– Kuchagua hotuba tofauti zilizotungwa na watu wengine na kuzitolea ufupisho.<br><br>– Kutambua vitenzi mbalimbali vilivyotumiwa katika hotuba, insha na vifungu vya ufupisho na |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kitenzi fulani viambishi zaidi vyenye kuusababishia maana mpya. | | – Mfano wa ufupisho (hotuba iliyotungwa hapo juu yaweza kuhusika)...<br><br>– Sarufi: uambishaji wa vitenzi | kuviambisha katika hali tofauti. |
| *Uhusiano wake na masomo mengine: Masomo yanayohusiana na kujenga mahusiano mema, kujenga tabia njema, umoja na ushirikiano, umoja na maridhiano, mapendo, adabu, siasa, dini, afya, n.k.* | | | | |
| *Vigezo vya tathmini au upimaji: Uwezo wa kutunga na kufupisha hotuba au tanzu nyingine za fasihi andishi ya Kiswahili.* | | | | |
| *Zana au vifaa: Vitabu , majarida, taarifa zilizorikodiwa, redio, runinga, simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati.* | | | | |

| MADA KUU | MADA NDOGO | |
|---|---|---|
| **iv.UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO** | **iv.MIDAHALO NA MIJADALA** | **Idadi ya vipindi: 62** |

**Ujuzi upatikanao katika mada:** Kuelewa mwongozo wa midahalo na mijadala na kushiriki katika kazi za majadiliano kwa kuzingatia mada zilizotolewa kujadiliwa; kujua jinsi ya kuchambua maneno ya Kiswahili kwa kutumia njia ya uambishaji.

| Malengo ya kujifunza | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Maarifa na ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | **Yaliyomo** | **Mbinu za kufundishia na kujifunza** |
| – Kutaja sifa au mwenendo unaofaa wakati wa kutoa hoja katika makundi.<br>– Kuelezea mazingira ya mada na kuijadili bila upotovu wowote.<br>– Kutambua lugha inayofaa katika majadiliano.<br>– Kutafsiri mtiririko wa hoja au majadiliano ili kujiepusha na marudio ya wazo au fikra.<br>– Kuonesha njia ya kutumia katika uambishaji wa maneno ya Kiswahili. | – Kutofautisha pande zinazoshiriki kwenye mdahalo au mjadala (mtetezi au mpinzani).<br>– Kutoa suluhisho katika majadiliano kwa kutetea hoja zinazomkera.<br>– Kutumia lugha sahihi na yenye kuvutia na kuridhisha.<br>– Kutumia ishara za mwili kulingana na hoja inayohusika.<br>– Kutoa hitimisho kwa kuzingatia maoni tofauti yaliyotokea pande mbili, | – Kuonesha moyo wa heshima wakati wa majadiliano.<br>– Kutokata tamaa na kutokasirika ovyo.<br>– Ushirikiano<br>– Urafiki<br>– Kujiamini. | – Sifa za mdahalo au mjadala.<br>– Mwongozo wa mdahalo/mjadala<br>– Mfano wa mdahalo na mjadala kuhusu athari za mavazi ya leo katika kuunga mkono tabia za uzinifu nchini.<br>– Sarufi: Uambishaji wa maneno ya Kiswahili. | – Kwa njia ya mijadala, wanafunzi wazungumzie mada zihusuzo masuala ya jamii kama vile: Rushwa, madawa ya kulevya, unyanyasaji wa kijinsia, desturi ya kujitegemea, kazi za umuganda katika maendeleo ya nchi, ndoa nchini Rwanda, malezi ya jana na ya leo, uzalendo (Ndi Umunyarwanda), ugonjwa wa ukimwi, n.k.<br>– Wanafunzi wapewe |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | yaani upande wa utetezi na upande wa upinzani... | | | zoezi la kusikiliza mijadala kwenye redio au kwenye runinga au vipindi vingine vya habari katika Kiswahili na kutoa ripoti kwa njia ya mazungumzo kufuatia pande mbili zilizohusika (upande wa upinzani na upande wa utetezi).<br><br>– Wanafunzi wapatiwe vifungu tofauti vya taarifa ambavyo ndani yake vitabeba maneno yalioambishwa na kuyachambua kwa kuonyesha njia iliyotumiwa katika uambishaji wake. |
| *Uhusiano wake na masomo mengine: Masomo ya kujenga ushirikiano, umoja na ushirikiano, adabu, n.k.* | | | | |
| *Vigezo vya tathmini au upimaji: Uwezo wakushiriki kwenye mdahalo au mjadala na kutoa hoja akimheshimu mpinzani wake.* | | | | |
| *Zana au vifaa: Redio, runinga, taarifa zilizorikodiwa, vifaa vya kunasia sauti, simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati, mtandao wa intaneti.* | | | | |

## 6. MAREJEO

F.E.M.K Senkoro (2011), *Mfululizo wa Lugha na Fasihi kitabu cha kwanza*, Kampuni ya Utamaduni, Tafsiri na Uchapishaji (KAUTTU).

Mkurugenzi, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (2004), Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la Pili, OXFORD University Press East Africa and Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, DAR-ES-SALAAM.
Makala za Semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili I (1983/2003), Fasihi, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo kikuu cha Dar es salaam

NIYOMUGABO C. (2013), *Mafunzo ya Kiswahili, kitabu cha Mwanafunzi* (Kidato cha 6), Fountain Publishers Rwanda Ltd.

Wizara ya Elimu (2010), *Muhtasari wa Somo la Kiswahili kidato cha 4*-6, Taasisi ya Taifa ya Ukuzaji mitaala ( NCDC).

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2005), *Muhtasari wa Kiswahili kwa Shule za Msingi Darasa la I-IV*, Taasisi ya Elimu Tanzania.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2009), *Muhtasari wa Kiswahili kwa Elimu ya Sekondari Kidato cha I-IV*, Taasisi ya Elimu Tanzania.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2009), *Muhtasari wa Kiswahili kwa Elimu ya Sekondari Kidato cha I-VI*, Taasisi ya Elimu Tanzania

## **7. VIAMBATANISHO:** MGAWANYO WA VIPINDI KWA MICHEPUO HUSIKA

| **Subject** | **Weekly period in S 4** | **Weekly period in S5** | **Weekly period in S6** |
|---|---|---|---|
| Mathematics | 7 | 7 | 7 |
| Physics | 7 | 7 | 7 |
| Computer | 7 | 7 | 7 |
| Chemistry | 7 | 7 | 7 |
| Geography | 7 | 7 | 7 |
| History | 7 | 7 | 7 |
| Economics | 7 | 7 | 7 |
| Literature in English | 7 | 7 | 7 |
| Kinyarwanda major | 7 | 7 | 7 |
| Kiswahili major | 7 | 7 | 7 |
| Religion major | 7 | 7 | 7 |
| Entrepreneurship | 6 | 6 | 6 |
| General studies and communication skills | 3 | 3 | 3 |
| English minor | 4 | 4 | 4 |
| French minor | 4 | 4 | 4 |
| Kiwahili minor | 4 | 4 | 4 |
| Kinyarwanda minor | 4 | 4 | 4 |